# MKUHUMI KWA AJILI YA JAMII NA MISITU TANZANIA WILAYA YA KILOSA



## KUSUDIO LA MRADI NI NINI?


Kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na madiliko ya tabianchi. Mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya jamii na uhifadhi wa misitu unatekelezwa kwa majaribio katika wilaya za Kilosa na Lindi vijijini. Lengo ni kuthibitisha katika ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa, njia ya kupunguza ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu kwa kutoa motisha wa kifedha wenye usawa kutoka soko la kimataifa la Kaboni kwa ajili ya jamii zinazosimamia au kuhifadhi misitu kwa njia endelevu katika ngazi ya jamii ya Tanzania. Mradi huu umefadhili na Serikali ya Norway kupitia wizara ya mambo ya nje.

## JINSI GANI JAMII INAWEZA KUNUFAIKA NA MRADI HUU?

- Kupata motisha wa kifedha kwa kuuza hewa ya kaboni/hewa ukaa.
- Kuboresha kilimo kwa kutoa elimu ya kilimo bora.
- Jamii/vijiji vitawezeshwa kuanzisha usimamizi shirikishi wa misitu hivyo kufaidika na rasilimaali za misitu.
- Jamii/vijiji vitawezeshwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo itapelekea vijiji kupata cheti cha kusimamia ardhi ya kijiji.
- Kujengea uwezo wanajamii kupitia mtandao wa MJUMITAkwa sasa bado halina msingi unaoeleweka.

## MRADI WA MKUHUMI UMETEKELEZWAJE KILOSA?

MKUHUMI kwa ajili ya jamii na hifadhi misitu Tanzania unatekelezwa katika vijiji takribani 22 (Vijiji 16 vipo ndani ya wilaya ya Kilosa na vijiji 6 vipo wilaya ya Mpwapwa). kama inavyoonyeshwa kwenye ramani




*Ramani inayoonyesha vijiji ambavyo vimo ndani ya mradi katika wilaya ya Kilosa na Mpwapwa.*

## SHUGHULI GANI AMBAZO MRADI UMETEKELEZA KATIKA NGAZI YA KIJIJI?

- Kuunda kamati za maliasili za vijiji.
- Kuwezesha vijiji.
  Kuandaa mipango ya Matumizi bora ya ardhi ya vijiji.
- Kuwezesha vijiji kuanza mchakato wa usimamizi shirikishi wa misitu.
- Taarifa za awali za msingi kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini.
- Kuandaa dira ya maendeleo ya vijiji kwa ajili ya utekelezaji MKUHUMI kama mkakati wa kukabiliana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu.
- Maandalizi ya Mkakati wa kuboresha kilimo.
- Tathmini ya visababishi vya ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu.
- Mafunzo ya awali kuhusu Usimamaizi Shirikishi wa Misitu, MKUHUMI na mabadiliko ya tabianchi.
- Mafunzo ya elimu ya mazingira mashuleni na MKUHUMI kwa walimu wa shule za msingi na waratibu wa elimu wa kata.



## MKUHUMI NI NINI?

MKUHUMI ni Mpango au Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa itokanayo na Ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa Misitu. Mpango huu ulianzishwa na nchi zilizoendelea kama njia moja wapo ya kutoa motisha ya kifedha kwa wahifadhi misitu katika nchi zinazoendelea. Mpango huu umebeba dhana kuu tatu za kimsingi ambazo ni ongezeko, uvujaji na hali ya kudumu.

### Ukataji wa miti ovyo ni nini?

Ukataji wa miti ovyo au kufyeka misitu ni ubadillishaji wa kudumu ardhi yenye misitu kwenda eneo lisilo na msitu.

### Je uharibifu wa misitu ni nini?

Mabadiliko ndani ya msitu ambayo huathiri vibaya muundo au utendaji wa eneo la msitu na hivyo kupunguza uwezo wa kutoa mazao ya misitu au huduma nyingine (Lakini hatimaye msitu hubaki kama msitu).

### Ongezeko

Ongezeko ni shughuli ambazo ni ongezeko kwenye shunghuli zinazoendelea tayari au
zilizopangwa zinakidhi kufikiriwa kupata malipo ya Kaboni. Kwa hiyo mdai lazima athibitishe kuwa shughuli hizi zisingefanyika kwa kutokuwepo mfumo wa soko la kaboni.

### Uvujaji

Uvujaji ni ongezeko la kiwango cha ufyekaji au uharibifu wa misitu kinachotokea nje ya mpaka wa mradi na ambayo inasababishwa na shughuli za mradi.

### Hali ya kudumu

Hali ya kudumu ni dhana inayohusiana na muda wa matokeo ya shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## MPANGO SHIRIKISHI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI NI NINI?

Mpango Shirikishi wa Matumizi Bora ya Ardhi ya kijiji ni mwongozo unaotokana na utaratibu wa kuwezesha wanakijiji kufanya maamuzi ya matumizi mbalimbali ya ardhi ya kijiji kwa kuzingatia utaalam.



## USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU NI NINI?

Usimamizi Shirikishi wa Misitu ni njia ya kusimamia misitu kwa uendelevu ambapo majukumu ya kusimamia misitu yanawekwa katika ngazi ya jamii, kundi au watu binafsi. Kuna njia mbili za Usimamaizi Shirikishi wa Misitu kwa Tanzania ambazo ni Usimamizi Misitu wa Jamii (CBFM) na Usimamizi wa Pamoja wa Misitu (JFM).

Vijiji vya Kilosa vilivyo kwenye mradi wa MKUHUMI vinatumia mfumo wa Usimamizi Misitu wa Jamii (CBFM) ambapo wanajamii ndio wana mamlaka yote ya kumiliki, kuusimamia na kutumia rasilimali zilizopo kwenye msitu kwa asilimia mia moja.

## CHANGAMOTO

- Wanakijiji waliofia kuwa watanyanganywa mashamba au makazi yao kuwa sehemu ya hifadhi.
- Wavunaji wa mazao wa misitu kama mbao na uchomaji wa mkaa walianza kuwashawishi wananchi wakatae mradi.
- Jinsi ya kuwaelezea wananchi soko la hewa ya ukaa ambalo kwa sasa bado halina msingi unaoeleweka.
- Maeneo mengi ya mradi hayafiki kwa urahisi kwahiyo kunahitaji kutembea kwa miguu kwa muda mrefu kufikia kijiji au kitogoji.
- Uchomaji wa moto kwenye maeneo ya misitu.

## NI NINI AMBACHO TUMEJIFUNZA?

Kutekeleza mradi wa MKUHUMI unahitaji ridhaa ya wananchi kutoka kwenye makundi yote hasa kupitia mikutano katika ngazi ya vitongoji. Pia wananchi wanahitaji mafunzo na uhamasishaji wa mara kwa mara kuhusu MKUHUMI kwani ni dhana mpya.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

**KUHUSU TFCG:** Dira ni kuona ulimwengu ambao Watanzania na wanadamu wengine wanafurahia manufaa mbalimbali yanayotokana na misitu yenye bioanuwai mwingi na inayosimamiwa na kuhifadhiwa vizuri.
**KUHUSU MJUMITA:** Dira ni kuona jamii ya Watanzania inayo jali, kulinda na kutumia misitu na raslimali inayotokana na misitu kiuendelevu.

Tunashirikiana na wadau kama Care Tanzania, TNRF Clinton Foundation, IRA, SUA, Halmashauri ya Wilaya na Wanajamii

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
MJUMITA

**Imetolewa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) wakishirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi Misitu Tanzania (MJUMITA).**
**TFCG, S.L.P 23410, Dar es Salaam, Tanzania. Barua pepe tfcg@tfcg.or.tz au MIJUMITA, S.L.P 21522 Dar es Salaam. Barua pepe: mjumita@googlemail.com**